# HALMASHAURI YA MJI GEITA

## KIZIDUO MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO TAREHE 15/11/2021.

**A: MKURUGENZI.**

1. Zahara M. Michuzi - Mkurugenzi - Mwenyekiti

**B: WAKUU WA IDARA WALIOHUDHURIA.**

1. Ndugu Thecla Gasembe - Mkuu wa Idara ya Utumishi - Katibu.
2. Ndugu K.S Katikiro - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara.
3. Ndugu Lucy D. Lyaruu - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya jamii.
4. Ndugu Leonard Chacha - Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji.
5. Ndugu Jasson B. Mutayabarwa - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi.
6. Ndugu Pius F. Magoti - Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji.
7. Mwl.Rashid Muhaya - Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari.
8. Ndugu Zenaida Alphonce - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi.
9. Eng.Oswald C. Mtei - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi.
10. Dr.Emmanuel Siro - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya.
11. Ndugu Barbara Mustafa - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipangomiji.
12. Ndugu Aloys I. Mutayuga - Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira.

**C: WAKUU WA VITENGO WALIOHUDHURIA.**

1. Ndugu Koshuma Ngoma - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi.
2. Ndugu Robert R. Matungwa - Mkuu wa Kitengo cha Sheria.
3. Ndugu Lee Joshua - Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki.
4. Ndugu Thomas N. Festus - Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA.
5. Ndugu Utali Makwea - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi.
6. Ndugu Method J. Lily - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi.

**D: WATAALAM MBALIMBALI WALIOHUDHURIA.**

1. Ndugu Upendo Kilonge - Mratibu TASAF.
2. Ndugu Mariam John - Mratibu wa Ukimwi.
3. Ndugu Zengo Polle - Afisa Maendeleo ya vijana.
4. Ndugu M.B Mathew - Afisa Utumishi.
5. Ndugu Violet I. Kiiza - Mkaguzi wa shule.

**E: SEKRETARIETI.**

1. Ndugu Renatus Samson - Mwandishi wa Vikao
2. Ndugu Kisabo E. Shineneko - Mwandishi wa Vikao

**MUHT. CMT.NA.1/11/2021.**
**KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwaarifu wajumbe kuwa akidi imetimia, kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao rasmi.

Mwenyekiti aliwakaribisha wataalam katika kikao hicho na kuwataka kuwa huru kutoa michango ya mawazo kwa manufaa ya Halmashauri ya Mji Geita.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua kikao rasmi saa 4:10 Asubuhi.

**MUHT. CMT.NA.2/11/2021.**
**KUTHIBITISHA DONDOO ZA AJENDA YA KIKAO.**

Dondoo zilizokubalika na kujadiliwa katika kikao hicho ni hizi zifuatazo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha dondoo za ajenda ya kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 16/10/2021.
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe 16/10/2021.
5. Taarifa ya mapato na matumizi kipindi cha mwezi Oktoba ,2021.
6. Maombi ya Tshs. 83,737,678.00 mabadiliko ya vifungu kwenda Akaunti ya Timu.
7. Kuwasilisha deni la kiasi cha Tshs. 310,313,600.00 la wafanyabiashara wa soko la dhahabu.
8. Taarifa ya mapokezi ya fedha za uviko-19 kiasi Tshs 1,220,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 61 kwa shule za sekondari na msingi
9. Taarifa ya mkaguzi wa ndani kipindi cha robo ya kwanza kutoka Julai hadi Septemba,2021.
10. Taarifa ya mabadiliko ujenzi wa uwanja wa mpira Magogo kutoka kwenye nyasi asili kuwa nyasi bandia.
11. Taarifa ya utekelezaji mradi wa Machinjio ya kisasa Mpomvu.
12. Kuwasilisha rasimu ya mpango wa motisha Halmashauri ya Mji Geita.
13. Kusudio la kutunga sheria ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya mji wa Geita za mwaka 2021.
14. Mapendekezo ya mfumo wa kutumia magari na matrekta yanayobeba taka.
15. Shughuli ya uhamasishaji na uchanjaji wa mbwa na paka.
16. Mpango wa kuanzisha kampuni ya Halmashauri.
17. Taarifa na Matangazo kwa idhini ya Mwenyekiti.
18. Kufunga kikao.

**MUHT. CMT.NA. 8/11/2021.**

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO - 19 KIASI TSHS 1,220,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 61 KWA SHULE ZA SEKONDARI NA MSINGI.**

Mkuu wa idara ya elimu sekondari aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za uviko - 19 kiasi cha Tshs. 1,220,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ambapo shule 17 za sekondari na shule moja ya msingi zimepokea fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 59 vya madarasa, kwa shule za msingi vyumba viwili na sekondari ikiwa ni jitihada za kuwezesha kupokea wanafunzi darasa la kwanza na kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2022.

Aidha alifafanua kuwa fedha hizo zimepokelewa katika akaunti za shule tarehe 21.10.2021 kwa maelekezo ya TAMISEMI utekelezaji ambao utafanyika kwa kipindi cha siku 60 kutoka tarehe 21.10.2021 hadi tarehe 21.12.2022. Kukamilika kwa madarasa hayo kwa wakati serikali itakuwa imefanikiwa kupokea wanafunzi wote bila changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa kipindi cha mwaka wa masomo 2022.

Hivyo mapokezi ya fedha za uviko - 19 zimefafanuliwa katika jedwali lifuatalo kwa kubainisha kiasi cha fedha kilichopokelewa na idadi ya vyumba vya madarasa kama ifuatavyo:-

| JINA LA MRADI | JINA LA KITUO/SHULE | IDADI YA MIUNDOMBINU(MADARASA) | KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA NA SERIKALI KUU | KIASI CHA FEDHA KILICHOPOKELEWA NA S/KUU | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | NYANKUMBU | 2 | 40,000,000.00 | 40,000,000.00 | Hatua za manunuzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | LUKARANGA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | KIVUKONI | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | NYANGUKU | 2 | 40,000,000.00 | 40,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | SHANTA MINE | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | MGUSU | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | NYABUBELE | 2 | 40,000,000.00 | 40,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | MKANGALA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | KASAMWA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | NYANZA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | IHANAMILO | 3 | 60,000,000.00 | 60,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | BUNGWANGOKO | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | BULELA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | MWATULOLE | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | KISESA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | KALANGALALA | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari | BOMBAMBILI | 4 | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | Hatua za manunuzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shule ya Msingi | ISENI | 2 | 40,000,000.00 | 40,000,000.00 | Hatua za manunuzi |

Baada ya kuwasilishwa taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya Uviko – 19 kutoka serikali kuu Timu ya Menejimenti walipokea na kusisitiza matumizi ya fedha hizo uwepo usimamizi lakini pia uwajibikaji wa hali ya juu kwa kushirikiana na uongozi wa shule zikiwemo bodi za shule, kamati za ujenzi kama ilivyofafanuliwa katika maelekezo kutoka TAMISEMI ili kuwezesha ujenzi kukamilika kwa wakati katika kufanikisha adhima ya serikali kupokea wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2022.

**UHT. CMT.NA. 18/11/2021.**
**KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wataalam kwa michango yao ya mawazo hadi kufikia mwisho wa kikao.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifunga kikao rasmi saa 2.50 usiku kisha kuwatakia wataalam usiku mwema.

**UMETHIBITISHWA**

**JINA**...Lee Joshua...... **JINA**...THECLA . G....

.............................. ..............................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**TAREHE**...22.12.2021...... **TAREHE**...22.12.2021......